# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA.

Shule ya Sekondari Mtande,
S.L.P. 167,
**CHUNYA.**

Kumb. Na. MSS/JI/29/ 14 **05/12/2020**

Mzazi/ Mlezi wa Mwanafunzi

..................................................

S.L.P....

**CHUNYA.**

**YAH. MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI MTANDE, 2021.**

1.0. Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2020. Shule ya sekondari Mtande ipo katika kijiji cha Mamba umbali wa mita 400 hivi kutoka barabarani. Muhula wa masomo utaanza ***tarehe 11/1/2021*** hivyo mwanafunzi anatakiwa aje tarehe hiyo ***saa 02:00 asubuhi*** tayari kwa kuanza kusoma.

**2.0. SARE YA SHULE NA MAHITAJI MENGINE**

**2.1. SARE**

a) Sare ya shule hii ni suruali/sketi mbili ( moja rangi ya damu ya mzee na nyingine ni kijani kibichi). Maelezo ya mshono ni: mifuko iwe ya kawaida isiwe mbele wala nyuma kwa wavulana na sketi ndefu mpaka kwenye kifundo cha miguu na ya malinda ya kawaida kwa wasichana.

b) Sare ya michezo kwa shule hii ni Track suit moja ya rangi nyeusi na raba za michezo kwa wasichana na wavulana

c) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi (viwe jozi 2).

d) Soksi jozi 2 nyeusi kwa wavulana na nyeupe kwa wasichana.

e) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi kwa wavulana.

f) Sweta mbili (moja rangi ya bluu iliyokolea na nyingine rangi ya kijani kibichi) kwa wote.

g) Mashati mawili meupe mikono mifupi.

h) Tai mbili (moja rangi ya kijani kibichi na nyingine rangi ya damu ya mzee).

i) **Tshirt za rangi ya njano** zenye nembo ya shule kwaajili ya muda wa kazi za kujitegemea (E.K)

### 2.2 VIFAA VYA DARASANI/MASOMO KWA MWANAFUNZI

i. Daftari kubwa 12
ii. Penseli na kalamu za kumtosheleza mwanafunzi
iii. Rula na mkebe mmoja
iv. Ndoo ya lita kumi(10) na ufagio mmoja kwa ajili ya usafi wa mazingira
v. Mfuko wa kubebea madaftari
vi. Faili moja kwaajili ya kutunzia kumbukumbu zake.

### 2.3 MAHITAJI MENGINE

i. Picha (passport size) akiwa amevaa shati jeupe

MUHIMU: Kwa mahitaji ya chakula na mengineyo *kamati ya wazazi* na *wazazi wenyewe* watakaa na kupeana utaratibu.

3.0 Viambatisho na Fomu muhimu

a) Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na mganga wa hospitali ya Serikali mara tu afikapo shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi kuhusu kutofanya fujo, mgomo na kutojihusisha na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri na kukubaliana na sheria na utaratibu wa shule kuhusu kumhudumia mwanae.
d) Mwanafunzi aje cheti cha kuzaliwa.
e) Mwanafunzi pia apewe/ akatiwe bima ya afya

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA.


MIKOMANGWA, M.F.
0625 732 594
Mkuu wa Shule
Makamu mkuu wa shule 0625447451
MKUU WA SHULE
MTANDE SEKONDARI
CHUNYA

# SHULE YA SEKONDARI MTANDE

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria Na-25 ya mwaka 1978. aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:

a). Heshima kwa viongozi, wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

b). Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.

c). Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (kwa walioko jirani na shule).

d). kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa

e). Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

f). Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.

g). Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa kulingana na utaratibu uliopangwa

h). Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

g). Kutii bendera ya Taifa

### MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Uasherati,ubakaji na ushoga
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
4. Uvutaji bangi
5. Makosa ya jinai
6. Kupigana na kupiga
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
8. Kudharau Bendera ya Taifa
9. Kuoa au kuolewa
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule na ukuadi.
11. Kutoa mimba
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu na kutukana matusi.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi
14. Kukamatwa / kutumia simu

## OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
## HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA.
### *FOMU YA KUKUBALI*

1. Mimi .................................................mvulana/msichana, nimekubali kujiunga kidato cha kwanza, 2019 katika shule ya sekondari Mtande tarehe ............................. nitafika shuleni bila kukosa ama kuchelewa, na nitasoma kwa bidii.
2. Nitatii sheria za shule, sitajihusisha wala kuchochea mgomo shuleni. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo, nidhamu na kazi za kujitegemea.
3. Sahihi ya mwanafunzi................................ Tarehe..................

**SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**

1. Mimi.................. Nimekubali mtoto wangu............asome katika shule ya sekondari Mtande kuanzia.......................

2. Ninaahidi kumpa vitu vyote anavyotakiwa kuwa navyo shuleni kama ilivyotajwa katika barua

3. Ninakuhakikishia kwamba nitamwonya mtoto wangu kutii sheria za shle na kuishi maisha mazuri na kuwa na bidii kwenye masomo na kazi za kujitegemea

4. Ninakubali mtoto wangu asome katika shule ya sekondari Mtande kama mwanafunzi wa kidato cha kwanza na ataendelea hivyo hadi atakapo maliza kidato cha nne.

5. Anwani yangu ya kudumu ni:

..................................................................

..................................................................

..................................................................

Sahihi........................... Tarehe ................

Fomu hii ijazwe na watu wa karibu wa mwanafunzi:

| Namba | Jina la ndugu | Mahali anakoishi | Namba ya simu | Kazi yake |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

MTANDE SECONDARY SCHOOL,

P.O. BOX 167,

**CHUNYA.**

**15/12/2019.**

TO MEDICAL OFFICER,
……………………………………
……………………………………
……………………………………..

**PART A.**

***REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION***

Please examine ……………………………………………………. (Name of student) to his/her fitness for pursuing further education at this school.

…………………………………

**HEAD MASTER**

1. Haemoglobin ……………………………………………………………………
2. P.V. bleeding ……………………………………………………………………
3. Sight ……………………………………………………………………………
4. Blood Pressure……………………………………………………………………
5. Urine for sugar …………………………………………………………………
6. Stool for routine examination ……………………………………………………..
7. Asthma ……………………………………………………………………………
8. Skin disease ………………………………………………………………………
9. Leprosy ……………………………………………………………………………
10. Any deformity……………………………………………………………………
11. Epilepsy ………………………………………………………………………...
12. Pulmonary tuberculosis…………………………………………………………
13. Neurosis …………………………………………………………………………..
14. General diseases …………………………………………………………………

**PART B:**

***(To be completed by a Government Medical Officer)***

I have examined the above named pupil and consider that he/she is physically fit and mental fit/unfit to join the school.

………………………..

Signature (Dr.)